Wassira amhakikishia Dkt. Samia 5 mingine ..Uk.3

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvinews@gmail.com

GAZETI LAKO

# JAMVI LA HABARI

ISSN Na 2683 - 6548: Toleo Na. 2520 ALHAMISI FEBRUARI 06, 2024 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

MIAKA 48 YA CCM

# DODOMA ZIMEZIMWA ZOTE IMEWASHWA CCM

>> **Dkt** Samia awaambia Wana CCM wasiwaogope wapinzani ila wasiwadharau

>> **Aahidi** kuimarisha Jumuia ya Umoja wa Vijana ili kupata viongozi imara

>> **Asisitiza** kupambana na tatizo la ajira kwa kuboresha Sera ya Elimu

Uk.2




## Dk. Mwinyi awataka wana CCM wahakikishe ushindi

Uk.2

# DODOMA ZIMEZIMWA ZOTE IMEWASHWA CCM

NA MWANDISHI WETU

SHEREHE za Chama cha Mapinduzi (CCM) kutimiza miaka 48 jana zililifunika kwa shangwe Jiji la Dodoma, kwa sherehe kubwa, ambapo mwenyekiti wake ambaye pia ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan alikuwa mgeni rasmi.

Akizungumza katika sherehe hizo, Dkt Samia alianza kwa kutoa rai kwa wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba huku akiwaondoa hofu dhidi ya wapinzani, lakini bila kuwadharau.

Rais Samia aliyasema hayo katika sherehe hizo ambazo ni rasmi kwa kuhitimisha kilele cha sherehe za CCM kutimiza miaka 48, zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, ambapo pia alizishukuru Jumuia za chama hicho za UVCCM, UWT na Sekretarieti ya chama kwa hamasa pamoja na maandalizi ya mkutano huo. Mwenyekiti huyo alikiri kuwa CCM ni chama imara na kina mtaji mkubwa wa wanachama ambao mpaka sasa wanafikia milioni 12 pamoja na wapenzi wengi, lakini alisisitza kuwa hiyo isiwe sababu ya kubweteka kwa mafanikio hayo na badala yake wanatakiwa kupambana ili kuwatumikia Watanzania ili waione thamani ya chama kilichopewa ridhaa ya kuongoza serikali yao.

"Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri," alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Vilevile katika hotuba yake mwenyekiti huyo ametilia mkazo kuimarisha Jumuia ya Vijana UVCCM, ambao ameitaja kuwa ndiyo itakayojenga chama imara kwa kuandaa viongozi wajao watakaokiendeleza chama hicho na baadaye kushika hatamu za uongozi.

Kuhusu ajira kwa vijana, Dkt Samia alisema tayari wameanza kuboresha sekta ya elimu wezeshi ambayo inatoa fursa kwa vijana kusomea mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri pamoja na kuwaajiri wenzao, pia masuala ya utalii, uchumi wa bluu pamoja na elimu ni miongoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima Agosti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti wa CCM, Mzee Steven Wasira akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzania, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.

Vilevile sherehe kama hizo zimefanyika maeneo mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Ruvuma ambapo

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa huo, Oddo Mwisho alisema, uamuzi ya kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais wa Tanzania na Dkt Hussen Mwinyi kupeperusha bendera ya chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka huu ni sahihi kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya kwa Watanzania.




# WASSIRA AMHAKIKISHIA DKT SAMIA 5 MINGINE

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Mzee Steven Wassira jana alitimiza siku 17 tangu Mkutano Mkuu ulipomchangua kushika nafasi ya kuwa makamu mwenyekikti wa CCM Bara na tayari ameshafanya ziara katika mikoa mitatu ya Dar es Salaam, Dodoma, Geita na Mara ambako kote amejiridhisha kuwa chama hicho kitashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Makamu huyo mwenyekiti aliyasema hayo alipokuwa akizungumza katika mkutano wa kilele cha maamdhimisho ya kutimiza miaka 48, CCM zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.

Alisema kuwa idadi kubwa ya Watanzania kwa dhati wanaonyesha imani yao kwa CCM na hasa Rais wake wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan kutokana na utekelezaji wake wa ilan za CCM pamoja na kutatua kero mbalimbali za wananchi.

"Kuna chombo Cha habari kilinipigi simu kikaniuliza kama tumeshaanza kampeni nikamwambia hapana ila tunatesti mitambo, napenda kusema kuwa sasa mitambo ipo tayari," alisema Mzee Wassira.

Alisema CCM inaongoza kwa ridhaa ya wananchi na Rais Dkt Samia ametekeleza ilani hivyo si rahisi kutokea kwa kuzuia 'mitano' tena kwake alisema.

# DK MWINYI AWATAKA WANA CCM WAHAKIKISHE USHINDI

NA MWANDISHI WETU

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amewataka wana CCM kuhakikisha chama hicho kinaendelea kushika dola katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama inavyoelezwa katika Katiba ya CCM.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana alipohudhuria kilele cha maadhimisho ya miaka 48 ya CCM, yaliyofanyika katika Uwanja wa Jamhuri, jijini Dodoma, aliwapongeza viongozi, wanachama, na wapenzi wa CCM kwa mafanikio makubwa yaliyojiri katika kipindi hicho cha miaka 48.

"Kwa hakika, wanaCCM tunayo kila sababu ya kufurahi na kujivunia mafanikio makubwa ambayo chama chetu kimeyapata. Sote tunawajibika kuyadumisha mafanikio haya kwa kuimarisha umoja na mshikamano. Tunakabiliwa na uchaguzi mkuu mwishoni mwa mwaka huu, hivyo ni jukumu letu kuhakikisha chama chetu kinaendelea kushika dola," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, Dk. Mwinyi alisisitiza umuhimu wa kuwaandikisha wanachama wote katika daftari la wapiga kura na kuwahamasisha kwenda kupiga kura wakati wa uchaguzi, ili kuhakikisha CCM inashinda na kuendelea kushika dola.

"Watanzania wanaamini kauli ya muasisi wa Taifa letu, Hayati Baba wa Taifa [Julius Nyerere] aliposema; bila ya CCM imara nchi yetu itayumba, hivyo hatuna budi kuhakikisha kwamba chama chetu kinaendelea kuwa imara ili nchi yetu isiyumbe na izidi kupiga hatua za maendeleo," alisisitiza Dk. Hussein Mwinyi.

# Kauli ya Dk Samia iliyowapa machozi watoto Jenerali

NA MWA NDISHI WETU

WAKATI Rais Samia Suluhu Hassan akiitaka Mahakama kutenda haki kwa usawa na wakati, watoto wa aliyekuwa Jenerali Tumainieli Kiwelu wanaomba shauri lao la kuondolewa kwa wasimamizi wa mirathi ya baba yao lililofunguliwa Mei,2024 limalizike.

Rais Samia akiwa kwenye maadhimisho ya wiki ya Sheria nchini alisema Mahakama ni muhimili muhimu wa kutenda haki kwa usawa na wakati huku ikichagiza shughuli za kiuchumi.

Shauri hilo la kuomba kuondolewa kwa wasimamizi wote watatu wa mirathi ya Jenerali Kiwelu lilifunguliwa Mei 21, 2024 na kupewa namba 11987/2024 mbele ya Hakimu Mkazi Eric Rwehumbiza wa Mahakama ya Wilaya ya Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Walalamikiwa katika shauri hilo ni watoto watoto watatu kati ya tisa wa Jenerali Kiwelu ambao walishindwa kutimiza wajibu wa kuzitambua, kuzikusanya na kuzigawa mali za marehemu baba yao kwa zaidi ya miaka mitatu sasa.

Licha ya kukaa kimya muda mrefu, wasimamizi hao wanalalamikiwa kwa kutumia baadhi ya mali bila kiwashirikisha watoto wengine wa marehemu hali inayoongeza hofu ya utapanyaji wa mali hizo kwa faida ya wachache walioaminiwa na Mahakama kupewa usimamizi wa mirathi.

Hata hivyo Desemba 5,2024 Hakimu Rwehumbiza alisoma uamuzi wa Mahakama na kuahidi kutoa ufafanuzi wa uamuzi huo na nakala ifikapo Februari 06,2025.

Jenerali Kiwelu alifariki Dunia Mei 18,2021 ambapo kabla ya kifo chake aliihudumia nchi hii katika nyadhifa mbalimbali ndani na nje ya jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) akishika nafasi za ukuu wa mikoa mitano tofauti.

# TRA, kariakoo waanza kutekeleza agizo la Dkt Samia

NA MWANDISHI WETU

BAADA ya Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt Samia wiki iloiyopita kutembelea eneo la Kariakoo, kwa ajili ya kukutana na wahanga waliopoteza ndugu zao kufuatia ajali ya kuanguka ghorofa, pia kuwapongeza waliohusika na kazi ya uokoaji, pia alizungumzia mkakati wa serikali kuboresha ukusanyaji kodi kwa wafanyabiashara wa eneo hilo.

Aligusia kuwa katika eneo hilo kuna matukio mengi ya ukwepaji wa kulipa kodi, hivyo akaagiza Maamlaka ya Mapato TRA kubuni mbinu rafiki zitakazowawezesha kukusanya kodi rafiki na walipa kodi.

Hivyo basi katika kuhakikisha wafanyabiashara wa soko kuu la kimataifa Kariakoo wanapata huduma zao karibu, Mkuu wa wilaya ya Ilala, Mkoani Dar es salaam Edward Mpogolo, amesema halmashauri hiyo ipo tayari kushirikiana na mamlaka nyingine ikiwepo TRA.

Mpogolo ameyasema hayo jijini Dar es salaam wakati wa Mkutano kati ya viongozi wa halmashauri, Kamishna Mkuu wa TRA YUSUPH MWENDA na jumuia ya wafanyabiashara Kariakoo.

Mpogolo amezungumza juu ya mikakati waliyojiwekea na wafanyabiashara wa Kariakoo wakiwepo machinga kufanya soko ilo kuwa rafiki na mazingira yenye kuleta faida kwa mlipa kodi.

Ameeleza nia njema ya wafanyabiashara endapo watakuwa katika mazingira rafiki ya kibiashara wanauwezo wa kulipa kodi, kuliko wanavyofanya sasa katika mazingira finyu ya barabarani.

Mpogolo ametumia nafasi hiyo kumshukuru Rais Dokta Samia Suluhu Hassan kwa kutowa fedha, kiasi cha shilingi bilioni 28 kwa ajili ya ujenzi wa soko jipya la kimataifa kariakoo, baada ya kuungua moto kwa soko la awali.

Huku shukrani nyingine kwa ajili ya Rais kutoa fedha za ujenzi wa soko jipya Jangwani, litalobeba wafanyabiashara wadogo, na kumtaka afisa biashara kuandaa kazi data ya wafanyabiashara walioopo kariakoo hivi sasa ili soko linapokamilika wapewe kipaombele na kuondoa malalamiko ya kukosa nafasi.




Mkuu huyo wa wilaya ya Ilala, Edward Mpogolo amemuhakikishia kamishna Mkuu wa TRA YUSUPH MWENDA, ofisi yake iko tayari kutoa ushirikiano kwa jumuia ya wafanyabiashara kariakoo, pamoja na jumuia ya wafanyabiashara Dar es salaam, kwani serikali inatambua namna walivyoweza kutoa ajira kwa watu wengi na kulipa kodi.


Hali iliyomfanya Mpogolo kuwataka wafanyabiashara ambao hawamo katika umoja wajiunge ili waweze kusaidiwa kirahisi changamoto zao kupitia viongozi wao, na kunufaika na umoja kwa kutambuliwa rasmi.

Kwa upande wake Kamishna Mkuu wa TRA YUSUPH MWENDA, amebainisha mchango mkubwa wa wafanyabiashara Kariakoo kwa kuzalisha walipa kodi wakubwa, wa kati na wadogojambo ambalo TRA inajivunia.

Kamishna huyo wa TRA amebaimisha mipango mitatu ya kuhakikisha umuhimu wa soko na wafanyabiashara Kariakoo moja wapo ni kuzalisha mabilionea wazawa na si kuzalisha mabilionea wageni kupitia soko hilo.

Nao wafanyabiashara wa soko la Kariakoo wamesema wako tayari kulipa kodi, ili wafanye biashara zao kwa amani wakati TRA imebainisha iko tayari kugharamia zoezi la kupata kazi data kwa wafanyabiashara wa Soko la Kariakoo waweze kutambulika rasmi.

# SAMIA, MWINYI WAMLILIA AGAKHAN




NA MWANDISHI WETU

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi wametuma salamu za rambirambi kufuatia kifo cha Kiongozi wa kiroho wa madhehebu ya Ismailia duniani na mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan.

Rais Samia amesema amepokea kwa huzuni taarifa ya kifo cha Mwanamfalme Karim Al-Husseini, Aga Khan IV.

"Kwa niaba ya Serikali na Wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, napenda kutoa rambirambi zetu za dhati na za moyoni kwa familia ya Mwanamfalme Karim, Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan, na Jumuia ya Waislamu wa Ismailia," amesema.

Rais Samia amesema Tanzania inaungana na jumuiya hiyo kuomboleza kifo cha kiongozi huyo mashuhuri na mwenye maono, ambaye kazi yake imegusa na kubadilisha maisha ya mamilioni ya watu kote ulimwenguni na kwamba fikra na maombi ya Watanzania yako nao katika kipindi hiki kigumu.

Kwa upande wake Rais Mwinyi amesema kwa niaba ya Serikali na Watu wa Zanzibar, anatoa pole kwa familia ya kiongozi huyo, Jumuia ya Waismailia, na wote walioguswa na alama aliyoacha.

"Tunapoomboleza msiba huu mkubwa, pia tunasherehekea kiongozi ambaye mazuri aliyofanya katika maisha yake yataendelea kuhamasisha vizazi vijavyo," amesema Rais Mwinyi.

Aga Khan amefariki dunia huko Lisbon, Ureno akiwa na umri wa miaka 88.

KIONGOZI Mkuu wa 49 wa Madhehebu ya Shia Ismailia na mwanzilishi wa Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), Mtukufu Aga Khan, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 88 jijini Lisbon, Ureno, Februari 4, 2025.

Mtukufu Aga Khan, anayefahamika kama Karim Al-Hussaini Aga Khan IV, alijulikana kwa mchango wake mkubwa katika kuboresha ustawi wa binadamu kupitia miradi mbalimbali duniani.

"Katika maisha yake, Aga Khan IV alisisitiza Uislamu ni imani inayohimiza kujitolea, uvumilivu, na utu wa mwanadamu," inasema taarifa rasmi kutoka Ureno.

Alizaliwa Desemba 13, 1936, Geneva, Uswisi, na alikulia Nairobi, Kenya. Alipata elimu katika shule ya Le Rosey nchini Uswisi na Chuo Kikuu cha Harvard, Marekani, ambako alisomea masomo ya Uislamu.

Baada ya kifo cha baba yake, aliacha ndoto zake za soka na masomo ya uzamivu ili kuchukua wadhifa wa Imamu wa 49 wa madhehebu ya Shia Ismailia.

Mbali na uongozi wa kidini, alihimiza maendeleo ya jamii kupitia sekta za afya, elimu, habari, utamaduni, na ustawi wa jamii.

Alianzisha miradi kama Shule na Chuo Kikuu cha Aga Khan, Mfuko wa Maendeleo ya Kiuchumi wa Aga Khan (AKFED), na Mtandao wa Maendeleo wa Aga Khan (AKDN), ambao umeleta maendeleo katika afya, elimu, na uchumi, hasa Afrika Mashariki.

Nchini Tanzania, mchango wake unaonekana kupitia Mwananchi Communications Limited (MCL) na Hospitali za Aga Khan, huku nchini Kenya alianzisha Nation Media Group (NMG) na viwanda kadhaa.

AKDN imeleta mafanikio katika jamii barani Afrika, Asia, na Mashariki ya Kati kwa kusaidia maendeleo katika maeneo yaliyoachwa nyuma.

Uteuzi wa Imam wa 50 na mazishi Imam wa 50 wa urithi tayari ameteuliwa, na atatangazwa rasmi baada ya wasia wa Mtukufu Aga Khan IV kusomwa katika siku zijazo. Taratibu za mazishi zitatangazwa hivi karibuni.

Kifo cha Mtukufu Prince Karim Aga Khan IV kinahitimisha enzi ya uongozi wa kipekee na huduma kwa binadamu, lakini urithi wake wa maendeleo na ustawi wa kijamii unaendelea kuhamasisha vizazi vijavyo.



&&&

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe Judith Kapinga ametoa rai kwa wananchi kuunganisha huduma ya umeme wakati miradi mbalimbali ya umeme inapotekelezwa ili kuepuka gharama inayoweza kutokea pale miradi inapokuwa imekamilika.

Mhe. Kapinga ameyasema hayo leo Februari 05 2025 bungeni jijini Dodoma wakati akijibu swali la la Mbunge wa Tanga Mjini Mhe. Ummy Mwalimu aliyetaka kufahamu Serikali ina mkakati gani wa kuwaunganishia umeme wa gharama nafuu kwa Wananchi wa maeneo ya Pembezoni yenye sifa za Vijiji mkoani Tanga.

"Katika kurahisisha upatikanaji wa huduma ya umeme wa bei nafuu kwa maeneo ya pembezoni mwa Jimbo la Tanga Mjini, Serikali kupitia REA inaendelea kutekeleza Mradi wa Peri-Urban III", Amesema Mhe. Kapinga.

Ameongeza kuwa mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi OK Electrical kwa kuunganisha wateja kwa baadhi ya mitaa kwa gharama ya shilingi 27,000 ambapo mpaka sasa jumla ya wateja 1,302 wameshaunganishiwa huduma ya umeme. Mhe. Kapinga amesema maeneo ya Tanga Mjini yaliyosalia yapo kwenye mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji 15 vya kila Mbunge (HEP IIA) ambapo Jimbo la Tanga Mjini litapelekewa umeme kwenye mitaa 15.

Akielezea kuhusu Serikali kuanzisha utaratibu wa kuwaunganishia umeme wananchi kwa mkopo, Mhe. Kapinga amesema Serikali inatekeleza miradi mbalimbali ya umeme ili kuwafikia wananchi kwa gharama nafuu ya shilingi 27,000/-.

Mhe. Kapinga ameongeza kuwa TANESCO ilishawahi kuwaunganishia wananchi kwa kuwakopesha ambapo ilikutana na changamoto ya wananchi kutokuwa na utayari ya kulipa madeni yao.

Akijibu swali Mbunge wa Ilemela, Mhe. Angelina Mabula aliyetaka kufahamu mitaa ya Masenene, Kilabela, Bujingwa, Nyanguku, Butimba na Toronto itapatiwa umeme kutokana na kuondolewa katika mitaa 15 inayotekelezwa na REA kutokana na kuwepo kwa njia kubwa ya umeme.

Akijibu swali hilo Mhe. Kapinga amesema miradi ya vitongoji ni ya ujazilizi ambayo inajumuisha ujenzi wa miundombinu ya umeme kwenye maeneo ambayo yamepitiwa na njia kubwa ya umeme ambapo pamoja na mitaa hiyo itanufaika.

# SERIKALI YAWAITA WALIOPITA USAILI

NA MWANANGU NGEMBAH

IDARA YA Utumishi wa Umma iliyopo chini ya Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira, imewaita waombaji waliofaulu usaili wa nafasi za kazi mbalimbali kuchukua barua zao za kupangiwa vituo vyao ndani ya siku saba baada ya tangazo hilo.

Taarifa ya Tangazo hilo ilitolea juzi na Ofisi ya Rais Sekretaieti ya Ajira katika utumishi wa Umma.

"Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma anapenda kuwataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali waliofanya usaili kati ya tarehe 24-02-2024 na tarehe 17-01-2025 kuwa matokeo ya waombaji kazi waliofaulu usaili huo ni kama yalivyoorodheshwa katika tangazo hili,"ilisema sehemu ya tangazo hilo

Aidha, orodha ya majina hayo pia inajumuisha baadhi ya wasailiwa waliokuwa kwenye kanzidata (Database) kwa kada mbalimbali ambao wamepangiwa vituo vya kazi baada ya nafasi kupatikana.



Kadhalika, waombaji waliofaulu usaili wanatakiwa kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi katika Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma zilizopo katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Kwenye Majengo ya Dk. Asha Rose Migiro, Masjala ya wazi ndani ya siku saba kutoka tarehe ya tangazo hili na baada ya hapo barua ambazo hazitachukuliwa na wahusika zitatumwa kupitia anuani zao za Posta,"ilisema taarifa hiyo

Vile vile, waombaji kazi waliofaulu usaili na kupangiwa kituo cha kazi wanatakiwa kuripoti kwa Mwajiri katika muda ambao umeainishwa kwenye barua za kupangiwa kituo cha kazi wakiwa na vyeti halisi (Originals Certificates) za masomo kuanzia kidato cha nne na kuendelea ili vihakikiwe na mwajiri kabla ya kupewa barua ya Ajira.

Mbali na hilo kwa wale ambao majina yao hayapo katika tangazo hili watambue kuwa hawakupata nafasi au hawakufaulu usaili, hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

"Jambo la muhimu kwa wale wanaokuja kuchukua barua za kupangiwa kituo cha kazi wanapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi,"ilieleza taarifa hiyo

Ambapo vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na Kitambulisho cha Uraia, Hati ya kusafiria, Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi, Kitambulisho cha Mpiga kura au Leseni ya Udereva.


# TANGAZA NASI SASA

*Unatamani kukuza biashara yako kutoka hapo ilipo kuwa kubwa na yenye mantiki zaidi?*

- *Unatamani kuongeza kipato, uelewa na upana wa shughuli zako za kila siku?*
- *Je unataka kuwafikia wateja wako ndani na nje ya nchi kwa kiasi kikubwa ili kukuza biashara na huduma yako?*
- *Fahamu kwamba JAMVI LA HABARI na mitandao yake ya kijamii kama Youtube, Instagram, Facebook, Website na Twitter hutembelewa na maelfu ya wasomaji kila siku Duniani kote.*
- *Hivi unafahamu kuwa JAMVILAHABARI kwa sasa ni moja kati ya Media chache zinazo ongoza kwa kutoa taarifa sahihi na kwa wakati zinazotokea nchini na Duniani kwa ujumla?*

*TANGAZA SASA NA JAMVI LA HABARI KWA PUNGUZO KUBWA LA BEI UPATE MATOKEO YA HARAKA.*

*Kwa matangazo yote kama vile minada, kupotelewa kwa vyeti vya shule, matangazo ya makampuni, nafasi za kazi, zabuni za kazi, maonyesho, dawa za asili, taasisi za elimu, taasisi za dini na mengine mbalimbali mbali mbali.*

*Ni rahisi sana, wasiliana nasi kupitia Whatsap namba +255659555744 au tupigie katika +255743777778 au +255659555744 GHARAMA ZETU NISAWA NA BUREE JAMVILAHABARI; TUMECHAGUA KUKUHUDUMIA www.jamvilahabari.co.tz*

# 'The Global Goalkeeper Award' ni fahari kubwa kwa Tanzania

NA MWANDISHI WETU

HABARI zilizogonga vichwa vya habari juzi ilihusiana na Tuzo ya The Global Goalkeeper Award, aliyotunukiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu Hassan, ikiwa ni kutambua juhudi za Serikali anayoiongoza katika kupambana na masuala ya uwekezaji katika sekta ya afya.

Juzi Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, muda mfupi baada ya kupkea Tuzo hiyo, aliwaambia watanzania kuwa Tuzo hiyo Maalum ya Kimataifa ya The Global Goalkeeper Award inathibitisha kuwa dunia imetambua juhudi za Tanzania katika kuboresha huduma za afya, husan kupunguza vifo vya akina mama wajawazito na watoto chini ya miaka mitano.

Rais Dkt. Samia alisema kuwa serikali anayoiongoza imeweka mipango madhubuti na kuongeza jitihada zaidi ili kuhakikisha kuwa ifikapo mwaka 2030, Tanzania inavuka lengo la kimataifa la kupunguza vifo vya akina mama, watoto wachanga na watoto chini ya miaka mitano.

Mhe. Rais Dkt. Samia aliyasema hayo siku Jumanne Juzi, Tarehe 4 Februari 2025, alipowahutubia waandishi wa habari mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma, akitokea jijini Dar es Salaam, ambako alipokea tuzo hiyo maalum ya kimataifa.

"Tuzo hii ina maana kubwa sana. Dunia imetambua jitihada zetu katika kuboresha huduma za afya, hasa afya ya mama na mtoto. Miaka minne iliyopita, vifo vya akina mama wakati wa kujifungua vilifikia 556 kwa kila vizazi hai 100,000.

"Lakini kwa sababu ya uwekezaji mkubwa katika sekta ya afya—kujenga miundombinu, kununua vifaa tiba, kusomesha wataalamu na kuajiri wahudumu wa afya wa ngazi zote—tumeweza kupunguza vifo hivyo vya akina mama na watoto. Kwa akina mama, tumevishusha kutoka 556 hadi 104. Lengo la kimataifa kwa mwaka 2030 ni kufikia vifo 70 kwa kila vizazi hai 100,000. Kwa mwenendo huu, hakika tutafikia au hata kuvuka lengo hilo," alisema Rais Dkt. Samia na kuongeza:

"Kwa watoto chini ya miaka mitano, tumepunguza vifo kwa kiwango kikubwa. Hata hivyo, bado tunakabiliana na changamoto kwa watoto wachanga, ambao wengi wao hupoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali, zikiwemo matumizi ya dawa za kienyeji na kuchelewa kufika hospitalini. Vilevile, awali hatukuwa na vifaa vya kutosha kuokoa maisha yao, lakini sasa tumewekeza kwenye ununuzi wa vifaa hivyo, na kwa hakika hali itazidi kuimarika."

Akijibu maswali ya waandishi wa habari, Rais Dkt. Samia alisisitiza kuwa ingawa uongozi wake umechangia mafanikio haya, tuzo hiyo ni heshima kwa Watanzania wote, husan watumishi wa sekta ya afya katika ngazi zote, ambao kwa juhudi zao wanawezesha huduma za afya bora kuwafikia wananchi.

Tuzo ya Global Goalkeeper Award, inayotolewa na Taasisi ya The Gates, hutunukiwa kwa viongozi wanaochangia kwa kiasi kikubwa katika kuharakisha maendeleo kuelekea Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs). Rais Dkt. Samia amekuwa kiongozi wa kwanza barani Afrika kupokea tuzo hii, ikiwa ni uthibitisho wa mafanikio ya Tanzania katika mapambano dhidi ya vifo vya akina mama wajawazito na watoto wachanga.



# TAHARIRI

## Kwa hili CCM inastahili pongezi

WANACHAMA wa Chama Mapinduzi (CCM), sambamba na wananchi wote Tanzania wametakiwa kuwa makini na viongozi wenye tabia ya uchonganishi kwa kile walichodai baadhi yao kuchochea chuki inayoweza kuwatenganisha.

Hiyo ni kauli makini iliyotolewa na katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Taifa ndugu Amos Makalla wakati akizungumza na Wananchi na wanachama wa Chama cha Mapinduzi katika Viwanja vya Umoja ni nguvu kusini Pemba ikiwa ni muendelezo wa ziara yake ya Mikoa 6 Visiwani Zanzibar.

Makalla pia amesema kuwa Dkt Samia Suluhu Hassan na Dkt Hussein Mwinyi hawana ubaguzi wowote kwenye suala la kuwaletea maendeleo lakini wenzetu kila kukicha wanaweka fitina na hili kazi kwenu Wazinzabar kwa ujumla wakataeni Viongozi hao na wanasiasa hao kwa kuwanyima kura wakati Uchaguzi utakapofika na tuchague chama cha mapinduzi ambacho ndio kina wajibu wa kuyaleta.

Kauli hii haistahili kupita bila kupongezwa ndiyo maama sisi JAMVI LA HABARI tunaipongeza kwa vile imezingatia kuleta umoja mshikamano na maelewano baina ya Watanzania.

Tunasema hayo tukijua kwamba kipindi kijacho yani Mwezi Oktona nchi itaingia katika kinyang'anyiro cha Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na Madiwani hivyo wasioitakia mema nchi wanaweza kutumia nafasi hiyo kuingiza chuki na hasama baina ya wananchi.

Tunaamini kila aliyesikia rai hii iliyotolewa na chama tawala, atazingatia kwa vile nchi hii ina wanasiasa na wasio wanasiasa ambao wanahitaji amani na utulivu.


## BODI YA UHARIRI

Mhariri Mkuu - 0762 178 678
Idara Ya Matangazo/Masoko - 0743 777 778, - 0659 555 744
Idara Ya Usambazaji - 0676807684, - 0787 288 160

Gazeti hili hutolewa na **JAMVI MEDIA GROUP**
S. L. P 78862, Dar es Salaam
**Tel:** +255 676 807684, 255 743 777778
**Email:** jamvinews@gmail.com
www.jamvilahabari.co.tz




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) mgombea urais kwa tiketi ya CCM mwaka 2025, Dk. Samia Suluhu Hassan (kushoto) akiwa na Katibu Mkuu wa CCM na mgombea mwenza wa urais 2025, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi wakiwa kwenye sherehe za miaka 48 ya chama hicho katika Uwanja wa Jamhuri mkoani Dodoma, jana.*

UCHAMBUZI

## Ushindi wa CCM unatokana na utekelezaji wa ilani yake

NA MWANDISHI WETU

SIRI kubwa ya maandalizi ya CCM Kushinda uchaguzi Mkuu na kuendelea kushika Doila, ni utekelezaji wa Ilani ya chama hicho ambayo viongozi, waliopewa nafasi walibeba na kuifanyia kazi kila eneo.

Hilo ndilo linaloweza kuwafanya wagombea wa chama hicho akiwemo mgombea nafasi ya Urais Dkt Samia Suluhu Hassan pamoja na jopo la wviongozi wengine watakaopambania nafasi za Ubunge na Madiwani.

Tayari chama hicho kimefanya chaguzi za ndani kama vile ule uliohusisha Mkutano Mkuu wa CCM, ulimchagua Mzee Steven wassira kuwa Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Bara.

Wassura aliyekuwa nje ya madaraka ya kisiasa kwa muda mrefu kwa maneno yake mwenyewe alieleza kushangazwa na ushindi ule na akaahidi kuifanya kazi hiyo kwa uadilifu na unyenyekevu mkubwa, kama hatua ya kulipa fadhjila na heshima ile kubwa.

Pia mkongwe huyo akatabiri ushindi wa kishindo utakaokipata chama chake, mtaji mkubwa ukiwa ni utekelezaji wa Ilani na jinsi chama hicho kinavyoendesha siasa zake kwa njia ya uwazi na uwajibikaji.

Mkongwe huyo ameingia na Falsafa ya Umoja Maridhiano na Ushindi, kazi ambayo amewaahidi wajumbe waliomuamini kushika wadhifa huo kuwa ataifanya kwa bidii kubwa huku akiamini ni jukumu lenye baraka za Mungu.

Kwa tathmini nyepesi ya ushindi huu wa Wasira una maana kubwa kwa CCM kuekelea uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani utakaofanyika mwaka huu, mwezi Okttoba kwamba mtaji wake unaonekana umeongezeka

Ukichukulia kuwa CCM ndicho chama kinachoongoza nchini kwa kuwa na wanachama na wapenzi wengi kinaweza kutumia mtaji huo kumpa ushindi wa kishindo mgombea wake wa Urais na hata Wabunge na Madiwani.

CCM ina watu wengi hata isipohitaji kura ya wapinzani au watu wasiofungamana na siasa ya chama chochote bado wana uhakika wa kushinda hususa nafasi ya Urais pengine baadhi ya wabunge wachache wanaweza kupoteza viti kutokana na kutowafanyia vizuri wapiga kura wao katika kipindi kilichopita.

Mgombea wa CCM anasaidiwa na maendeleo yanayoonekana kila kona, atahitaji timu ya kawaida tu kumnadi na kuweza kumpa ushindi wa kimbunga kama huu alioanza kuonyesha dalili Mzee Wasira

Ushindi wa CCM mwaka huu unaonekana bila kuhitaji utafiti mkubwa, kwani hata ukiangalia upande wa upinzani bado unaonekana kama hakuna chama chenye nguvu kama ilivyokuwa katika chaguzi za awamu zilizoipita tangu kuanzishwa mfumo wa vyama vingi vya Siasa mwaka 1992

Licha ya CCM kujiandaa kama ilivyokuwa wakati wote inapoingia katika uchaguzi, lakini mwaka huu licha ya uwepo wa maridhiano ya kisiasa, lakini upinzani unaonekana kupoteza nguvu kuliko miaka yote ya uchaguzi.

Ni mwaka tutakaoendelea kusikia vishindo vya CCM katika majimbo na makelele ya wapinzani watakaoendeleza msamiati wa kuibiwa kura ili hali hawakuwa na maandalizi zaidi ya malumbano na kukashifiana.

# Dk Samia: Wapinzani tus

NA MWANDISHI WETU



MWENYEKITI WA Chama Cha Mapinduzi Dkt Samia Suluhu Hassan, ametoa rai kwa wanachama wa chama hicho kujiandaa kwa kampeni za Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba huku wakiondoa hofu dhidi ya wapinzani, lakini bila kuwadharau.

Aliyasema hayo alipokuwa akihutunbia katika kilele cha sherehe za CCM kutimiza miaka 48, zilizofanyika katika Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma ambapo pia alizishukuru Jumuia za Chama hicho UVCCM, UWT na Sekretarieti ya chama hicho kwa hamasa pamoja na maandalizi ya mkutano huo.

Mwenyekiti huyo alikiri kuwa CCM ni chama imara na kina mtaji mkubwa wa wanachama ambao mpaka sasa wanafikia Milioni 12 pamoja na wapenzi wengi, lakini alisisitza kuwa hiyo isiwe sababu ya kubweteka kwa mafanikio hayo na badala yeke wanatakiwa kupambana ili kuwatumikia Watanzania ili waione thamani ya chama kilichopewa ridhaa ya kuongoza Serikali yao.

“Tunataka watupime kwa tunachokifanya leo, watuchague kwa sera pamoja na mipango mizuri” alisema Dkt Samia huku akishangiliwa na umati wa Wana CCM pamoja na wapenzi wa chama hicho waliohudhuria sherehe hizo.

Vilevile katika hotuba yake Mwenyekiti huyo ametilia mkazo kuimarisha Jumuia ya vijana UVCCM, ambao ameitaja kuwa ndiyo itakayojenga chama imara kwa kuandaa viongozi wajao wataokiendeleza chama hicho na baadaye kushika hatamu za uongozi.

Kuhusu Ajira kwa vijana Dkt Samia alisema, tayari wameanza kuboeresha Sekta ya Elimu wezeshi ambayo inatoa fursa kwa vijana kusomea mafunzo ya ufundi ili waweze kujiajiri pamoja na kuajiri wenzao, pia masuala ya utalii, Uchumi wa Bluu pamoja na elimu ni miongoni mwa mambo yanayotiliwa mkazo ili kuwakomboa vijana katika tatizo kubwa la ukosefu wa ajira linaloikumba dunia hivi sasa.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, mwenyekiti huyo alisisitiza matumizi ya teknolojia hiyo kwa maendeleo, huku akitoa mfano jinsi yeye mwenyewe alivyoweza kuwatumia ujumbe wanachama wengi akiwataka wajitokeze kwenda kupiga kura katika uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika nchi nzima Mwezi Agisti mwaka jana na kufanikisha chama chake kushinda kwa kishindo.

Sherehe kama hizo pia zilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini, huku Wana CCM wakijipongeza kwa kuwa ni chama imara kinachoendelea kuaminiwa na wananchi na kushika Dola kwa miaka mingi.

Awali Makamu Mwenyekiti Mzee Steven Wasira akizungumza katika sherehe hizo alisema, CCM kinaendelea kuongoza kutokana na kupata ridhaa ya Watanzaniua, hivyo amewataka wale wanaosema chama hicho kimekaa sana madarakani, waeleze kama kuna ahadi au mipango ya muda ambayo walikaa na kupangiana kutawala kwa zamu.

Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea heshima.


Vilevile sherehe kama hizo zimefanyika maeneo mbalimbali ukiwemo mkoa wa Ruvuma ambapo

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi mkoa huo Oddo Mwisho alisema, uamuzi ya kuwapitisha Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea Urais wa Tanzania na Dkt Hussen Mwinyi kupeperusha Bendera ya Chama hicho katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu ni sahihi kutokana na mambo makubwa waliyoyafanya kwa Watanzania.

Mwisho, amewataka Wak
wa Mkoa wa Ruvuma kutemb
kifua mbele kutokana na mae
deleo makubwa yaliyopatika
katika kipindi cha miaka min
ya uongozi wa Rais Dkt San
Suluhu Hassan.

Aidha,amewasisitiza Waka
wa Mkoa huo kutumia mu
wao kujikita kwenye shugh
za uzalishaji mali hasa kilin
kwani Serikali imewekeza ng
vu kubwa kwa kutoa pembe
za ruzuku bure kwa Wakulin
ili kuongeza uzalishaji na kule
tija kwa Wakulima.

# siwaogepe, tusiwadharau



> Alisema tangu alipochaguliwa kushika nafasi hiyo jana ikifikia siku ya 17, ameshakutana na watu wengi na kupata uhakika wa jinsi CCM ilivyojijengea

Katika hatua nyingne Mwisho,amewaagiza maafisa kilimo na maafisa Ushirika Mkoani Ruvuma, kuhakikisha wanatenda haki kwenye suala la ugawaji wa pembejeo kwa kuhakikisha kila mkulima ananufaika na matunda ya Serikali yake badala ya kugawa pembejeo hizo kwa upendeleo.

Pia,amewakumbusha Wanachama wa Chama hicho kutimiza wajibu wao kwa kueleza mambo mazuri yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ili Wananchi wafahamu maendeleo yaliyofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika kipindi cha miaka minne badala ya kukaa kimya.

Amewashukuru Wananchi wa Wilaya ya Tunduru kwa maamuzi sahihi kwa kuwachagua wagombea wa CCM kwenye Uchaguzi wa Serikali za mitaa uliofanyika mwaka uliopita ambapo Chama hicho kilipata ushindi wa kishindo.

Mkuu wa Wilaya ya Tunduru Simon Chacha alisema,katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan wamepokea zaidi ya Sh.bilioni 300 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kwa mujibu wa Chacha,fedha hizo zimetumika kutekeleza miradi maj i,elimu,afya,umeme,Barabar a,Mawasiliano,Utumishi na Utawala Bora na kuwezesha Wananchi wa Wilaya ya Tunduru kupata huduma bora za kijamii,kisiasa na Kiutamaduni.

Alisema,Sh.bilioni 5,598,853,033.85 zimetumika kujenga miundombinu ya vyumba vya madarasa,maabara za sayansi,mabweni,miundombinu ya vyoo na maji kwenye shule za Sekondari na Sh.bilioni 2,545,934,950.50 zimetumika kujenga miundombinu kama hiyo katika shule za msingi.

Katika sekta ya afya alisema,wamepokea Sh.bilioni 3,155,923,169.67 kujenga zahanati,vituo vya afya,nyumba za Watumishi,miundombinu ya vyoo na maji na Sh.bilioni 1,106,017,026.21 zimetumika kwenye mpango wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia mapato ya ndani(mikopo ya asilimia kumi).

Aidha,Halmashauri ya Wilaya imetumia Sh.bilioni 11,346,151,952 kuwezesha mpango wa kunusuru kaya maskini(Tasaf) ,elimu bila malipo kwa shule za Sekondari,ujenzi wa miundombinu shule za msingi(BOOST)na pembejeo za kilimo.

Alisema,Wakala wa maji na usafi wa mazingira vijijini(Ruwasa) umepokea Sh.8,271,911,919.52,TARURA Sh.bilioni 10.500,Mamlaka ya maji Tunduru mjini Sh.bilioni 3.9,Tanesco Sh.bilioni 10.490,umeme vijijini(REA)Sh.bilioni 11.984 na miundombinu ya umeme Imara Sh.bilioni 245.980.

Naye Katibu Tawa la wa Wilaya ya Namtumbo Fransis Mgoloka alisema,katika kipindi cha miaka minne Wilaya hiyo imepokea zaidi ya Sh.bilioni 46.554 kati ya hizo Sh.bilioni 3.351 zimekwenda kwenye sekta ya afya,elimu Sh.bilioni 9, Sh.bilioni 8 umeme vijijini(REA) na sekta ya maji Sh.bilioni 7.8.






# MFUMO WA 'MODULI' KUPOKEA RUFAA KIELETRONIKI UMEZINDULIWA



NA MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Fedha Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.), amezindua rasmi matumizi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa katika Mfumo wa Ununuzi wa Umma kwa njia ya Kieletroniki (NeST)

Dkt. Mwigulu amezindua rasmi matumizi ya moduli hiyo Jijini Mwanza wakati wa mafunzo ya moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko na rufaa (Complaint and Appeal Management Module) katika Mfumo wa NeST.

Katika Hotuba yake iliyosomwa na Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga amesema kuwa kuanza rasmi kwa matumizi ya moduli kuna faida kadhaa zikiwemo kuokoa muda, gharama, kupunguza mianya ya rushwa, kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa Umma.

"Moduli hii mpya inalenga kurahisisha zoezi zima la uwasilishaji wa malalamiko na rufaa kwa upande wa wazabuni na pia itawezesha taasisi nunuzi na Mamlaka ya Rufani kushughulikia Malalamiko na rufaa kupitia Moduli hii hivyo kupunguza muda na gharama zinazo ambatana na zoezi zima la utoaji wa haki," amesema Dkt. Mwigulu.

Dkt. Mwigulu alitoa rai kwa wazabuni wote nchini pamoja na taasisi nunuzi kuwa tayari kujifunza na kutumia Moduli ya kuwasilisha na kushughulikia malalamiko na rufaa kwa njia ya kielektroniki ili kuokoa muda na fedha ambazo zingetumika katika uwasilishaji na ushughulikiaji malalamiko na rufaa zinazotokana na michakato ya ununuzi wa Umma.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Mamlaka ya Rufani ya Zabuni za Umma (PPAA), Bw. James Sando amesema kuwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi Imara wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, PPAA imeweza kushughulikia mashauri 162 yaliyotokana na michakato mbalimbali ya Ununuzi wa Umma.

"Katika mashauri hayo, PPAA ilizuia utoaji tuzo kwa zabuni 35 zenye thamani ya takriban shilingi bilioni 583.6 kwa wazabuni wasio na uwezo wa kifedha pamoja na wale waliokosa sifa za kitaalamu za kutekeleza zabuni husika, amesema Bw. Sando.

Bw. Sando aliongeza kitendo cha kuzuia tuzo kwa wazabuni hao kiliiepusha Serikali kuingia katika mikataba ambayo ingepelekea kuwa na utekelezaji wa miradi usioridhisha hivyo kusababisha upotevu wa fedha za umma na kuchelewesha maendeleo stahiki kwa wananchi.

"PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa Umma nchini, imeweza kushiriki katika kutungwa upya kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2023 na Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2024, amesema Bw. Sando

Bw. Sando ameongeza kuwa, ili kuendana na mabadiliko yaliyoletwa na Sheria ya Ununuzi wa Umma, PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa Umma nchini, imeandaa Kanuni za Rufaa za Ununuzi wa Umma za mwaka 2024 ambazo zimetangazwa kwenye Gazeti la tarehe 31/01/2025 kupitia Gazeti la Serikali (GN no.65/2025).

Mafunzo ya matumizi rasmi ya moduli awamu ya pili kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa yametanguliwa na mafunzo ya awamu ya kwanza yaliyofanyika Mwezi Mei 2024 kwa mikoa ya kanda ya Pwani iliyojumuisha Dar es Salaam, Pwani, Tanga na Morogoro.

Kamishna wa Sera ya Ununuzi wa Umma, Dkt. Frederick Mwakibinga akiwasilisha Hotuba kwa wazabuni na Taasisi nunuzi kwa niaba ya Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba (Mb.) wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Matumizi rasmi ya Moduli ya kupokea na kushughulikia malalamiko kieletroniki kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa tarehe 04 Februari 2025, Jijini Mwanza.

> "PPAA kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na taasisi zinazosimamia ununuzi wa Umma nchini,



# WATENDAJI 7 WAPIGWA STOP RUVUMA

NA MWANDISHI WETU



BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya Mbinga Mkoani Ruvuma, limewasimamisha kazi Watendaji saba wa vijiji kwa upotevu wa Sh.milioni 28,236,400 kwa tuhuma za ubadhirifu wa zaidi ya Shilingi milioni 28 ambazo walikusanya kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya mapato vya Halmashauri kupitia mashine za POS na kushindwa kupeleka Benki fedha.

Maazimio ya kuwasimamisha kazi Watumishi hao yametolewa jana na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo Desderiue Haule mara baada ya Baraza kugeuka kuwa kamati ili kuwajadili Watumishi hao baada ya kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili taarifa za robo ya pili kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kilichofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri hiyo.

Alisema, Halmashauri iliunda Tume maalum ya kuchunguza upoteza huo na imebaini watendaji wametumia fedha hizo bila kufuata kanuni, taratibu na sheria za kuomba idhini ya kuhamisha fedha au kubadilisha matumizi kutoka kifungu kimoja kwenda kingine na kushindwa kufanya mrejesho katika Ofisi ya Mweka Hazina.

"Watendaji hao baada ya kufikishwa kwenye kamati ya maadili, Waheshimiwa Madiwani wameunga mkono hoja na mapendekezo ya tume ya uchunguzi na timu iliyoundwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmasahuri juu ya kuwasimamisha kazi na wanatakiwa kurudisha fedha hizo"alisema Haule.

Aidha, amempongeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Tume iliyochunguza suala la nidhamu kwa Watumishi hao ambapo ameagiza kuwasimamia ili waweze kurejesha fedha walizochukua.

Katika hatua nyingine Haule alisema, Baraza la Madiwani limemsimamisha Diwani wa Kata ya Mapera Betram Komba, kutohudhuria vikao vitatu baada ya kukutwa na hatia ya kukiuka maadili ya kikanuni kwenye vikao, kutoa lugha isiyokuwa staa na kufanya vurugu kwenye kikao.

Haule, amewapongeza Watumishi na Madiwani kwa kazi nzuri wanayofanya ya kuibua vyanzo vipya na kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani hali iliyowezesha Halmashauri hiyo kuwa kinara wa kukusanya mapato kati ya Halmashauri nane za Mkoa wa Ruvuma.

Kwa upande wake Afisa Rasilimali Watu wa Halmashauri hiyo Festo Mwangalika amewataja Watendaji hao na fedha walizoshindwa kupeleka benki ni Festho Komba(Sh.milioni 7,527,100) Mwajuma Matily (Sh.580,000) na Shaban Mkongo( Sh.582,000), Fotnatus Ngongi(2,626,000) Keneth Moyo(10,448,000) Sotely Kawhili(2,734,300) na Gaston Mbunda(Sh.3,739,000).

"Halmashauri imewasimamisha kazi kwanza ili wasiendelee na majukumu yao wakati uchunguzi wa suala lao unaendelea, lakini baada ya kuitwa kwenye kamati ya maadili baadhi yao wameanza kurejesha fedha walizochukua"alisema.

Mwangalika alisema, kosa la Watumishi hao ni kukusanya fedha bila kuzipeleka Benki jambo ambalo ni kinyume na sheria za Mamlaka ya Serikali ya mwaka 2009 na wamepewa muda wa miezi sita kurejesha fedha hizo na taratibu nyingine zilizopendekezwa na kamati zitatekelezwa juu yao.

# KAMPENI YA UIBUAJI WA WAGONJWA WA KIFUA KIKUU

NA MUHIDIN AMRI, TUNDURU

WIZARA ya Afya kupitia mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Ki kuu na Ukoma imesema, kampeni ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kiku u itawafikia watu wote walioba inika kuwa na maambukizi ya ugonjwa huo ambao hawakufikiwa mwaka 2024.

Watu hao, wataanzishiwa Dawa ha raka kwa ajili ya kuzuia uweze kano wa kuambukiza watu wengin e ili kuifanya Tanzania kuwa nchi salama bila kuwa na watu walioambukizwa ugonjwa wa kifua kikuu ifikapo mwaka 2 030.

Hayo yamesemwa jana na Mwakili shi wa Wizara ya Afya kitengo cha kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma Dkt Jacob Mwanamtwa, baada ya kukagua utekelezaji wa kampeni hiyo katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Tunduru Mkoani Ruvuma.

Alisema, Wizara ya Afya imejipa nga na itahakikisha inawapata wagonjwa ambao hawakupatikana mwaka 2024 na kuwaanzishia matibabu yanayotolewa bure kwenye vituo vya Afya na Hospitali zote hapa nchini.

"Wagonjwa ambao hawajapatiwa m atibabu wanaendelea kuambukiza watu wengine katika jamii yetu na mbaya zaidi mgonjwa ambaye hajaanza kutumia Dawa anaweza kuambukiza watu kati ya 10 hadi 15 kwa mwaka" alisema Dkt Jacob.

Alisema, wameanza kampeni hiyo kwenye mikoa tisa hapa nchini ambayo haikufanya vizuri katika kuibua wagonjwa wa kifua kikuu mwaka jana ikiwemo Mkoa wa Ruvuma na kupitia kampeni hiyo wagonjwa wote watafikiwa ili waweze kuanzish iwa matibabu.

Alisema, malengo ya Shirika la Afya Duniani(WHO) kutokomeza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030 , lakini kutokana na changamoto mbalimbali yanaweza yasifikiwe au yakafanikiwa kutokana na mikakati iliyowekwa na Serikali yetu kupitia Wizara ya Afya.

Mratibu wa Kifua Kikuu na Ukom a wa Wilaya ya Tunduru Dkt Mkasange Kihongole alisema, kupitia kampeni ya mpango harakishi watahakikisha wananchi wote wanapata elimu ya kifua kikuu, wanafanyiwa

*Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.*



uchunguzi na ambao watabainika kuwa na vimelea vya ugonjwa huo wataanzishiwa dawa.

"katika kipindi hiki cha mpito ambacho tunatakiwa kufanya kazi kwa juhudi kubwa tumeanza kuangalia maeneo hatarishi zaidi, baada ya hapo wataalam tutasambaa kwenye maeneo mengine ambayo siyo hatarishi lakini kuna watu ambao wako kwenye hatari ya kupata ugonjwa huo"alisema Mkasange.

Mkasange ametaja maeneo hatari shi ni kwenye maboma ya wafuga ji, vijiwe vya boda boda, wachez a bao, Pooltable machimbo ya madini na maeneo mengine yenye mikusanyiko ya watu kuanzia watano na kuendelea.

Aidha alisema, kabla ya Wizara ya Afya kuzindua mpango haraki shi wa kuibua wagonjwa wa TB, Wilaya ya Tunduru imeshaanza kutekeleza kampeni hiyo kwenye vijiji vyote vinavyozun gukwa na machimbo ya madini, shule za Msingi na Sekondari za bweni.

Mkasange alisema, walianza kamp eni ya uelimishaji, uibuaji na uchunguzi wa TB mapema ili kwenda na kasi ya mpango harakishi wa uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu iliyozinduliwa wiki iliyopita ili kukata mnyororo wa maambukizi katika wilaya ya Tunduru.

Naye Mratibu wa huduma za maab ara Mkoa wa Ruvuma Said Kaunde alisema, kampeni ya mpango harakishi ya uibuaji Wagonjwa wa Kifua Kikuu imegawanyika kwenye makundi mawili ambayo ni kuwafikia Wananchi wenye vimelea vya TB kwa ajili ya kuchukua sampuli za makohozi na kuwaanzishia Dawa.

Alisema, katika mkakati wa kuto komeza ugonjwa huo Serikali yetu imewekeza fedha nyingi kwenye vifaa tiba hasa kununua mashine za kisasa za uchunguz i wa vimelea vya kifua kikuu na katika Mkoa wa Ruvuma kuna mashine 11 ambazo zimepelekwa kwenye Halmashauri zote nane.

Pia alisema, tangu kampeni hiyo ilipoanza hadi sasa wamefanik iwa kukusanya sampuli zaidi ya 851 ambazo baada ya kupelekwa maabara kwa ajili ya uchunguzi,24 zimekutwa na maambukizi ya ugonjwa huo.

Muhudumu wa afya ngazi ya jami i Idd Yakiti(Nyuki) alisema, kwenye kampeni ya uibuaji wa Wagonjwa wa Kifua Kikuu kazi anayofanya ni kwenda kwenye zahanati ili kuchukua makohozi ya wahisiwa na kuzifikisha Hospitali ya wilay a kwa ajili ya uchunguzi.

Nyuki, ameipongeza Serikali kup itia Wizara ya Afya kwa kuchuk ua hatua katika kukabiliana na ugonjwa huo ambao ni miongoni mwa magonjwa kumi Ulimwenguni yanayoongoza kusababisha vifo vya watu wengi.



# WIMBO 'KAKA SELEMANI' WA MSONDO! UMETIMIZA MIAKA 48 KAMA CCM



NA MWANDISHI WETU

1973 ulikuwa mwaka mzuri kwa Bendi ya NUTA jazz, si wanamuziki pekee bali hata wafanyakazi wa Muungano huo wa Wafanyakazi walipagawishwa na ujio wa mwimbaji kijana sana aliyejiunga na bendi mwaka huo.

Huyo ndiye Hassan Rehani Super Stereo aliyejiunga na bendi hiyo awali akidharauliwa kutokana na umri wake, lakini pale alipokaribishwa jukwaani bendi ilitikisika

Alipotinga Dar akitokea Arusha kwa ajili ya majaribio aliikuta bendi inajiandaa kusafiri kwenda Dodoma.

Viongozi wakaamuru na Bitchuka naye awemo katika msafara huo wa Treni ili wakamjaribu kama atafaa au hatakuwa na tija.

Mwenyewe alikuwa na Siri kubwa moyoni, akijipanga kuwanyamazisha pindi watakapompa nafasi, pengine aliyekuwa akifahamu makjali yake ni kaka yake na rafiki Said Mabela waliowahi kufanya kazi pamoja Arusha Jazz.

Naam saa na dakika zikatimia bendi ikafika salama na muda wa usiku ikaanza kutumbuiza katika ukumbi wa Dodoma Hotel huku Bitchuka akifuatilia kila tukio.

Hatimaye muziki ukazimwa na kutangazwa uwepo wake pia akatakiwa kupanda jukwaani ili kusalimia kisanii.

Lilikuwa kosa kubwa kwani mwamba huyo alipokabidhiwa kipaza sauti akafanya balaa kubwa akiimba wimbo maarufu wenye maneno “Ukiwa kama hunitaki”

Sauti yake ya juu, jinsi alivyoweza kuimba kama pacha na mwimbaji kinara Muhimu Gurumo ilimpagawisha kila aliyekuwemo ukumbini pamoja na wanamuziki wenzake, aliposhuka jukwaani saa hiyo hiyo ikapigwa simu Dar es Salaam akiagizwa Boss kuandaa haraka mkataba wa kijana huyo.

Bitchuka akafikia kusaini na kuanza kazi pia akipewa nafasi ya kuachia kibao chake cha kwanza na yeye akaamua kurudisha shukran kwa mashabiki kwa kutunga kibao kiitwacho ‘Msondo wa NUTA’.

Kuanzia hapo kila aliyetaka kutunga wimbo basi pia alitamani kusikia Bitchuka akiimba na hiyo ikadumu kwa kipindi kirefu sana akiitumikia bendi hiyo kutoka 1917 hadi 1979 alipohamia Mlimani park.

Yote tisa, Kumi ni Katia tukio la bendi kutoka kuitwa NUTA na kuwa Juwata, baada ya kuunganishwa vuyama vya TANU na ASP mwaka 1977 bendi hiyo nayo mikakumbwa na mabadiliko hayo ya jina tu lakini wanamuziki ni walewale.

Wanamuziki wakapanga kutunga vibao hatari vitakavyoshabihiana na mabadiliko ya ya jina la bendi.

Naam ilipofika mwisho mwisho wa mwaka hupo Tarehe 11.11.1977 Mabrok Khalfan akatunga wimbo wenye mahadhi ya rumba na wenye miondoko ya taratibu pia akataka Bitchuka atambae katika sauti tamu ya Kwanza.

Wimbo huo ukawa katika albam yenye wimbo Nidhamu ya kazi ambao nao ulikuwa wenye viewango vya Lami.

Albam hii ilileta mtikisiko wa hali ya juu kwa mashabiki kuongezeka Msondo kiasi cha kuhitajika nguvu ili uweze kupata tiketi mapema ili uingia kufaidi midundo ya Msondo Ngoma.


Au ukizubaa utaingia ukumbini lakini hutoweza hata kuwaona wanamuziki.

Kutokana nyomi linavyojazana.

# Michezo Kimataifa




## Tetesi za soka




MANCHESTER United wameomba kufahamishwa kuhusu mustakabali wa mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa Christopher Nkunku, 27, huku winga wa Argentina Alejandro Garnacho, 20, akihusishwa na uhamisho wa kwingineko.



JUVENTUS wameipa Chelsea ruksa ya kumsajili kiungo wa kati wa Brazil Douglas Luiz, 26, ambaye pia ananyatiwa na Manchester City na Arsenal, hii imetokana na mazungumzo mazuri kati ya klabu hizo na pia maslahi yaliyoridhiwa na pande hizi mbili.




1

MSHAMBULIAJI wa Uingereza Marcus Rashford, ambaye amejiunga na klabu ya Aston Villa kwa mkopo, huenda asicheze tena Man United kwa vile uhusiano kati ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 na timu hiyo ya Old Trafford umesambaratika. (Guardian)

BAADA ya kulaulimiwa kwa muda mrefu kuwa tatizo la Arsenal ni kudharau kufaya usajili hasa eneo la ufungaji, hatimaye klabu hiyo imesikia kilio hicho na sasa imeanza mawindo makali ili kutibu pengo lililopo, kufutia mkakati huyo klabu hiyo imeingia chimbo na kumnasa Straika makali Raia Slovenia anayekipiga katika klabu ya RB Leipzig ya Ujerumani



## Rashford apunguza presha Aston Villa

NA HENRY PAUL

ASTON Villa wamefanikisha usajili wa mshambuliaji Marcus Rashford kutoka Manchester United.

Rashford alijiunga na Villa kwa mkopo wa miezi mine hadi Juni. Kwa mujibu wa taarifa ya mwandishi wa habari za usajili nchini Italia, Fabrizio Romano asilimia 70 ya mshahara wa Rashford utatolewa na Villa huku United ikitoka asilimia 30.

Mkopo huo una kipengele cha Rashford kuuzwa moja kwa moja Villa Park kwa uhamisho wa pauni milioni 40 kwa mkataba wa miaka mitatu na nusu. Villa wameomba vipimo vya afya vifanyike leo.

Villa wamemuuza mshambuliaji Jhon Durán kwenda Al-Nassr huku kukiwa na tetesi huenda Ollie Watkins akatimka pia, licha ya kocha wa Villa, Unai Emery kudai mwingereza huyo hauzwi. Villa pia wanakaribia kumnasa Marco Asensio kutoka PSG.

Awali Rashford alikaririwa akisema kuwa yuko tayari kwa changamoto mpya baada ya hivi karibuni kuibuka tetesi za nyota huyo kuachana na Mashetani Wekundu na kuondoka viunga vya Old Trafford alikodumu kwa takriban miaka 20

Rashford ambaye hakuwa sehemu ya kikosi cha United kilichoibugiza Man City 2-1 wikiendi iliyopita alimueleza mwandishi wa habari za michezo wa jarida la World soccer kuwa hana wasiwasi na yuko tayari kuondoka kwa wema ikiwa hahitajiki tena na United.

“Binafsi nadhani niko tayari kwa changamoto mpya, na ikiwa nitaondoka haitakuwa vita, hamtasikia ubaya wa Manchester United kutoka kwangu. Kama najua hali ni mbaya, sitaizidisha kwa kuongea. Nimeona namna wachezaji wengine wanavyoondoka na mimi sitaki kuwa wao nikiondoka taarifa nitatoa mimi” amesema Rashford.

Rashford amefunga mabao matatu tangu kocha mpya Ruben Amorim atwae mikoba ya kuinoa timu hiyo, na hivi karibuni alizomewa na mashabiki wa timu hiyo alipofanyiwa mabadiliko mapema katika kipindi cha pili cha ushindi wao wa 2-1 dhidi ya Viktoria Plzen kwenye Europa league

# Michezo Kimataifa




# DAVIES MWAPE ALIPELEKA MAJONZI MSIMBAZI 2011

NA HENRY PAUL

MIONGONI mwa matukio yaliyowahi kuwafurahisha wanachama na wapenzi wa klabu ya Yanga, moja ni lile la timu yao yenye maskani yake makuu Kariakoo, makutano ya mitaa ya Jangwani na Twiga, kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Mchezo huo ambao ulikuwa ni mkali na wa kusisimua kwa muda wote wa dakika 90, ulichezwa siku ya Jumamosi Oktoba 29, 2011, katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam (sasa Uhuru) na ulikuwa ni wa mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo ulianza kwa kasi, huku timu zote zikishambuliana kwa zamu. Yanga walikuwa wanashambulia na pindi Simba nao walipokuwa wanapata nafasi walikuwa wanashambulia pia.

Mabeki wa timu zote mbili walikuwa makini mno katika kudhibiti mashambulizi yaliyokuwa yakielekezwa langoni mwao, huku washambuliaji nao walikuwa wakifanya mashambulizi kadhaa wakiwa na lengo la kutaka kupata bao la mapema mapema.

Mashambulizi ya Yanga, yalikuwa yakiongozwa na Davies Mwape, Kenneth Assamoah na Amisi Kiza, huku mashambulizi ya Simba yalikuwa yakiongozwa na Felix Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe.

Kosa kosa za kutaka kufunga zilikuwa zikitokea pande zote mbili, kwa sababu mabeki walionekana kuwa imara katika kudhibiti mashambulizi ya washambuliaji.

Katika dakika ya 30 hivi, Simba walifanya shambulizi moja kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini shuti hafifu alilopiga Emmanuel Okwi, lilidakwa kirahisi na kipa wa Yanga Yaw Berko.

Yanga ilijibu shambulizi hilo katika dakika ya 32 hivi, baada ya kiungo wao mahiri Haruna Niyonzima kutoa pasi kwa Kenneth Assamoah, lakini shuti lake lilitoka sentimita chache langoni mwa timu ya Simba.

Dakika ya 40 hivi, Simba walifanya shambulio lingine kali langoni mwa timu ya Yanga, lakini Sunzu aliyecheza vizuri siku hiyo, alikosa bao la wazi baada ya kubaki yeye na kipa wa Yanga Berko, kwani shuti lake kali alilopiga lilitoka nje kabisa.

Hadi dakika 45 za kipindi cha kwanza zinamalizika, timu hizo zilikwenda mapumziko matokeo yakiwa ni suluhu ya 0-0.

Kipindi cha pili nacho kilianza kwa kasi, huku timu zote mbili zikifanya mabadiliko ya wachezaji wao. Katika dakika ya 50, Simba ilimpumzisha Amri Kiemba na nafasi yake kuchukuliwa na Haruna Moshi 'Boban'.

Kuingia kwa kiungo mashambuliaji 'Boban', kwa kiasi fulani kuliongeza kasi ya mashambulizi kwa upande wa Simba, kwani walionekana kufanya mashambulizi mengi langoni mwa timu ya Yanga tofauti na mwanzoni.

Yanga kwa kutaka kuongeza mashambulizi mbele, katika dakika ya 55, ilimtoa Amis Kiza na nafasi yake kuchukuliwa na Idrisa Rashid ambaye baada ya kuingia alioneza kasi ya mashambulizi kwa timu yake ya Yanga.

Dakika ya 70 hivi, Simba ilimtoa winga wa kushoto Ulimboka Mwakingwe na nafasi yake kuchukulia na Mwinyi Kazimoto.


Katika dakika ya 75 hivi, Yanga walifanya shambulio moja la nguvu langoni mwa timu ya Simba na kufanikiwa kupata bao la kuongoza ambalo lilifungwa na Davies Mwape.

Dakika ya 80 hivi, Yanga ilifanya badiliko lingine kwa kuingia Jerry Tegete aliyechukua nafasi ya mfungaji wa bao pekee Davies Mwape.

Pamoja na mabadiliko ya wachezaji kufanywa na pande zote, lakini hapakuwa na mabadiliko ya matokeo, hivyo hadi dakika 90 za mchezo zinamalizika, Yanga walitoka uwanjani wakiwa vifua mbele baada ya kumfunga mtani wake wa jadi Simba bao 1-0.

Kikosi cha Yanga: Yawa Berko, Godfrey Taita, Oscar Joshua, Chacha Marwa, Nadir Haroub 'Cannavaro', Juma Seif 'Kijiko', Nurdin Bakari, Haruna Niyonzima, Davis Mwape/Jerry Tegete, Kenneth Assamoah na Amis Kiza/Idrisa Rashid.

Kikosi cha Simba: Juma Kaseja, Said Nassor 'Chollo', Juma Jabu, Juma Nyoso, Victor Costa 'Nyumba', Jerry Santo, Amri Kiemba/Haruna Moshi 'Boban', Shomari Kapombe, Felex Sunzu, Emmanuel Okwi na Ulimboka Mwakingwe/Mwinyi Kazimoto.



JAMVI LA HABARI
SPOTI
ALHAMISI FEBRUARI 06, 2025



## Diamond aunguruma na live band CCM Dodoma

>> Soma Uk. 15

# KOCHA YANGA ATIMKA, WAMALIZA HASIRA KWA SINGIDA BIG STAR

## >> Yaichakaza Ken Gold mabao 6-1




NA MWANDISHI WETU

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Yanga Sead Ramovic jana kumalizia kibarua cha kuisimamia timu hiyo ya Jangwani ilipoumana na Ken Gold, katika Uwanja wa KMC na kupata ushindi mnono wa mabao 6-1.

Kwa mujibu wa taarifa zilizotoltwa na Klabu hiyo kongwe nchini, inasema kuwa, kocha huyo alivunja mkataba ghafla katika Klabu hiyo ya Wananchi, huku ikidaiwa anakwenda nchini Morocco alikopata kibarua cha kuinoa klabu ya CR Belouizdad iliyomtengea donge nono.

Juzi asubuhi Kocha Ramovic akiongea na Waandishi wa habari alisema kwamba ana kazi kubwa ya kuiongezea maarifa timu yake ili iweze kushinda kila mechi, iweze kutetea ubingwa wake lakini jioni yake mambo yakabadilika.

Wakati mashabiki wa Yanga wakiwa bado wanatafakari pigo hilo la kuodokewa na kocha wake ghafla habari zinabainisha kuwa aliyekuwa kocha wa Singida Black Stars, Hamdi Miloud Raia wa Algeria aliwasili Jijini fasta akitokea Singida tayatri kutwaa mikoba ya mtangulizi wake huyo, kuwatumikia wananchi.

# VAR yapunguza makosa uwanjani

NA MWANDISHI WETU

KUMEKUWA na makosa 13 ya waamuzi wasaidizi wa video (VAR) katika Ligi ya Premia hadi sasa msimu huu yakiwa ya chini kutoka 20 yaliofanyika katika hatua kama hiyo muhula uliopita.

Hatua nne zisizo sahihi za VAR na uingiliaji kati mara tisa uliofanyika kimakosa kutoka kwa mzunguko wa mechi za kwanza 23 zimegunduliwa na jopo la Matukio Muhimu ya Mashindano (KMI).

Kumekuwa na uingiliaji kati mara 70 wa VAR katika mechi 239 za ligi msimu huu - karibu moja katika kila mechi tatu. Ligi hiyo



inasema usahihi wa 'Matukio Muhimu ya Mechi' ni 96.4% - kutoka 95.7% katika hatua inayolingana muhula uliopita.

"Hakuna mtu anayedharau umuhimu na athari ya kosa moja," afisa mkuu wa kandanda Tony Scholes alisema.

"Tunajua kwamba kosa moja linaweza kugharimu klabu. Pointi na matokeo yanaweza kuathiri nafasi za wasimamizi, na nafasi za wachezaji ."

Katika kesi ya Erik ten Hag, hilo ndilo lililotokea - moja ya makosa manne ilikuwa adhabu iliyotolewa dhidi ya timu yake ya Manchester United katika mechi ambayo ilionekana kuwa mechi yake ya mwisho.




## Rashford apunguza presha Aston Villa

ASTON VILLA wamefanikisha usajili wa mshambuliaji Marcus Rashford kutoka Manchester United. Rashford alijiunga na Villa kwa mkopo wa miezi mine hadi Juni. Kwa mujibu wa..

>> Inaendelea Uk. 14

GAZETI HILI HUTOLEWA NA JAMVI MEDIA GROUP, S. L. P 78862, DAR ES SALAAM